ELIMU INAYOZINGATIA UMAHIRI

TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA WA 3 2026

GREDI YA 5

KISWAHILI LUGHA

MUDA: Dakika 40

JINA: _____NAMBARI YA AD: _____

SHULE: _____TAREHE: _____

MAAGIZO KWA WANAFUNZI

1. Karatasi hii ina **maswali 30 ya kuchagua jibu sahihi**.
2. **Jibu maswali yote.**
3. Kwa kila swali, chagua **jibu sahihi kati ya machaguo manne A, B, C na D**.
4. **Andika herufi pekee ya jibu sahihi** katika nafasi uliyopewa.
5. Soma kila swali kwa makini kabla ya kujibu.
6. **Usiandike jibu zaidi ya moja** kwa swali lolote.

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu swali.

Daktari: Pole kwa maumivu, Mzee. Karibu kiti ukae.
Mgonjwa: Asante, Daktari.

Daktari: Hebu nieleze, unaumwa wapi?
Mgonjwa: Ninaumwa na tumbo na kichwa.

Daktari: Pole sana. Shida hiyo ilianza lini?
Mgonjwa: Karibu wiki moja sasa.

Daktari: Je, unahisi maumivu unapokwenda haja ndogo?
Mgonjwa: Hapana, Daktari. Tumbo tu ndilo linauma.

Daktari: Sawa. Nitakutuma kwenye maabara ufanyiwe uchunguzi wa haja kubwa na ndogo.
Mgonjwa: Sawa, Daktari.

1. Mgonjwa anaumwa na nini?

A. Mgongo B. Kichwa C. Mkono D. Mguu

2. Mgonjwa alitumwa kwenye _____ kufanyiwa uchunguzi.

A. Hospitali B. Zahanati
C. Maabara D. Shule

3. Mgonjwa alianza kuwa na shida kwa muda wa muda gani?

A. Wiki moja B. Mwaka mmoja
C. Mwezi mmoja D. Wiki mbili

4. Mgonjwa alitumwa kwenye maabara kufanya uchunguzi wa _____.

A. Mkono B. Haja kubwa na ndogo
C. Mgongo D. Kichwa

5. Anayewatibu wagonjwa huitwa nani?

A. Muuguzi
B. Daktari